# MTIHANI WA DARASA LA TANO

# MWISHO WA MUHULA WA KWANZA

# 2019 KISWAHILI

***SOMA MAAGIZO HAYA KWA MAKINI***

*1. Hakikisha umeandika*

*(i)Jina lako* *(ii)Jina la shule yako*

***Muda: Saa 1 Dak. 40***

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Shule __1__ ina sifa kochokocho.Shule ya Johari ni __2__ sana. Mwanzo, shuleni Johari mna wanafunzi __3__ nidhamu. Walimu wetu wana bidii ya __4__. Wao hufundisha __5__. Sisi hushiriki katika __6__ mbalimbali. Mifano ni netiboli, voliboli na soka. Aidha wanafunzi hufaulu katika mitihani. Wanafunzi hao __7__ kwa hivyo, mtihani unapokaribia sisi __8__ kwa bidii sana. Tunajua kuwa __9__

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. letu | B. yetu | C. chetu | D. wetu |
| **2.** | A. nzuri | B. mzuri | C. zuri | D. kizuri |
| **3.** | A. chenye | B. zenye | C. yenye | D. wenye |
| **4.** | A. chawa | B. mchwa | C. nyuni | D. mbuzi |
| **5.** | A. vyema | B. njema | C. jema | D. chema |
| **6.** | A. mchezo | B. masomo | C. michezo | D. kazi |
| **7.** | A. huadhibiwa | B. hutuzwa | C. hupumsishwa | D. hukomeshwa |
| **8.** | A. hudurusu | B. hucheza | C. hulala | D. hukomeshwa |

**9.** A. mtoto akililia wembe mpe B. bendera hufuata upepo
C. mtaka cha mvunguni sharti ainame D. dunia hadaa ulimwengu shujaa

Maria alikuwa mwanafunzi mwenye __10__. Yeye alikuwa akifika shuleni __11__ na mapema. Hata hivyo, siku __12__ alikuwa amechelewa. Walimu walishangaa. Wanafunzi wenzake walikuwa na wasiwasi __13__ haikuwa kawaida yake. Kumbe Maria alikumbana na msongamano __14__ wa magari barabarani.Ajali ilikuwapo ndiyo maana Maria __15__ shuleni mapema.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **10.** | A. adhabu | B. nidhamu | C. hishima | D. ukaidi |
| **11.** | A. asubuhi | B. mchana | C. jioni | D. alasiri |
| **12.** | A. hii | B. hiyo | C. hilo | D. huyo |
| **13.** | A. lakini | B. ilhali | C. wala | D. kwa sababu |
| **14.** | A. mkubwa | B. kubwa | C. mdogo | D. kikubwa |
| **15.** | A. aliingia | B. hakuchelewa | C. alifika | D. hakuwasili |

***Kuanzia swali la 16 - 30, jibu kulingana na maagizo.***

**16.** Nomino muwa iko katika ngeli gani?

A. LI-YA B. I-ZI

C. U-I D. U-ZI

**17.** Tunasema gari;

A. mpya B. kipya

C. jipya D. lipya

**18.** Ni kipi kisichopatikna sebuleni?

A. rafu B. meza

C. kochi D. kitanda

**19.** Mtu akikuamkua kwa kusema :"hujambo" utajibu

A. hujambo B. hawajambo

C. sijambo D. salama



Compiled & distibuted by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

20. Vazi ambalo ni muungano wa suruali na shati si

A. surupwenye B. bwelasuti

C. ovarali D. kaptura

21. Kamilisha methali: Mpanda ngazi

A. huwa juu B. hupaa

C. hushuka D. hurudi

22. _______ nitaenda shuleni kesho.

A. Mimi B. Sisi

C. Wewe D. Yeye

23. Mstari mmoja wa shairi huitwa

A. kina B. mizani

C. ubeti D. mshororo

24. Ndege ni kwa kiota kama vile konokono ni kwa

A mzinga B. kizimba

C. zizi D kombe

25. **Andika kwa umoja**

Masikio haya yanauma

A. Sikio hili haliumi.

B. Sikio hili linauma.

C. Sikio hili kinauma.

D. Sikio hii inauma.

26. Nitamwitaje mtoto wa mtoto wangu?

A. kilembwe B. kitukuu

C. mjukuu D. mwanangu

27. Chakula ____ chumvi kali hakiliki.

A. chenye

B. yenye

C. zenye

D. lenye

28. Kwenye kikombe kile hakuna chai_________.

A. yote B. yoyote

C. chochote D. lolote

29. Ugonjwa unaoenezwa na mbu huitwa

A. mafua

B. kifaduro

C. malaria

D. malale

30. Mvua ilinyesha______ giza kuingia.

A. juu ya

B. baada ya

C. chini ya

D. mbele ya.

**Soma habari ifuatayo kisha ujibu maswali 31 – 40.**

Michezo ni shughuli muhimu katika maisha ya mwanadamu. Michezo ina manufaa mengi kwa binadamu. Michezo hufanya mwili wa binadamu kuwa imara na dhabiti. Mazoezi huimarisha baadhi ya viungo vya mwili wenyewe.

Mazoezi ya mwili pia hufanya akili zetu kuwa makini sana. Tukumbuke kuwa mazoezi , tunayofanya hutumia sehemu fulani ya akili na kwa hivyo kuifanya kuwa makini zaidi. Akili zinapokuwa makini, mtu huweza kufikiri na kuamua mambo kwa haraka na isitoshe, uamuzi wenyewe huwa ni wa kufana.

Michezo siku hizi ni kama kazi. Wanamichezo wengi hupata mkate wao wa kila siku kwa michezo kama vile kandanda, riadha, uendeshaji magari na tenisi miongoni mwa michezo mingine mingi.

Michezo pia inaweza kutumiwa kama njia ya kuunganisha watu kutoka jamii tofauti. Michezo huwa kama kiungo cha watu. Mbali na kuunganisha watu, michezo pia ni njia za kuhubiri amani na utangamano kati ya wananchi mbalimbali. Kwa kushiriki katika michezo mtu huweza kujua mengi kwa vile hutembea kwingi ni kuona mengi. Mtu huweza kutoka Kenya akaenda nchi mbalimbali za Afrika na pia Ulaya.



Compiled & distibuted by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com

Mwanachezo ni mtu anayeheshimika sana kutokana na nidhamu yake ya hali ya juu. Ni mtu mwaminifu na ambaye anaweza kutegemewa sana katika masuala mbalimbali.

Serikali yetu imetia bidii sana katika kuhakikisha kuwa michezo inapewa nafasi kubwa kuanzia shuleni na hata vyuoni. Serikali inawaomba wote wenye vipaji mbalimbali michezoni kujitokeza na kuvikuza ili nchi yetu iendelee kutia fora duaniani katika michezo.

---

**31.** Katika aya ya pili, mwandishi anasema kuwa michezo

A. huimarisha afya

B. hukuza elimu

C. huvutia maisha

D. hupendeza ulimwengu.

**32.** Michezo humwezesha mtu kufikiri

A. na makini

B. pa makini

C. kwa mkini

D. kwenye makini

**33.** Katika maisha ya sasa

A. michezo ni kama mshahara

B. michezo ni kama kazi

C. michezo ni kama shamba

D . michezo ni kama pesa.

**34.** Ni mchezo upi ambao haujatajwa katika kifungu?

A. ndondi B. kandanda

C. riadha D. tenisi

**35.** Michezo pia inaweza kutumika

A. kuunganisha watu

B. kutenganisha watu

C. kufukuza watu

D. kupiga watu

**36.** Kulingana na kifungu, mwana michezo hana sifa hii

A. mwaminifu B. mwenye adabu

C. mtiifu D. mzembe

**37.** Kwa nini mwanamichezo huheshimika;

A. ana nidhamu

B. ni mtukutu

C. ana misuli

D. ana marafiki wengi

**38.** Wanafunzi wanaoshiriki katika michezo wana uwezo wa

A. kufeli mitihani

B. kuwa watundu

C. kufaulu mtihani

D. kuwa wadogo

**39.** Serikali inawaomba wote wenye vipawa michezoni

A. kuwa wazembe

B. kutoshiriki michezoni

C. kuvikuza

D. kuvididimisha

**40.** Mchezo wa watoto wa kujificha na kutafutana unaitwa

A. kibe B. filiti

C. gongo D. jungwe

***Soma ufahamu ifuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50.***

Arusi ya Aisha na Juma **ilifana** mno kiasi cha kuvutia umati mkubwa sana wa watu. Siku yenyewe ilikuwa siku ya Jumamosi. Viongozi kutoka tabaka mbalimbali walikuwa wamefika ili kushuhudia hawa wawili wakifunga pingu za maisha. Siku hiyo hakika ilikuwa siku ya kipekee.

Arusi yenyewe ilichacha alasiri huku watu waking'ang'ania nafasi. Matayarisho yalikuwa swadakta na hata vijana wa Uswahilini walibeba wali kwenye mashati. Mara kwa ghafla akaja mama mmoja kwenye umri wa makamo na kujitambulisha kuwa mke wa Juma. Tulishangaa!

Watu wengi walipigwa na butwaa chakari na kubaki vinywa wazi wasijue la kufanya. Lakini kumbuka maajabu hayaishi. Dunia haiishi kwa mambo ya kustaajabisha.

**41.** Harusi ya Aisha na Juma ilifana. Huku ni kumaanisha
- A. ilichukiza
- B iliharibika
- C. ilipendeza
- D. ilitumbukia nyongo

**42.** Umati mkubwa wa watu pia huitwa
- A. halaiki
- B. thurea
- C. shungi
- D. genge

**43.** Ni usemi upi sahihi
- A. harusi ilipendeza mwanzoni
- B. Aisha na Juma walioana
- C. Aisha na Juma walikuwa maadui
- D. Juma alikuwa na bibi wawili

**44.** Kufunga pingu za maisha ni
- A. kufurahia
- B. kumfunga mtu pingu
- C. talaka
- D. kuoana

**45.** Arusi ilifanyika siku gani?
- A. Jumamosi
- B. Alhamisi
- C. Jumapili
- D. Alasiri

**46.** Ni nani aliyepigwa na butwaa?
- A. maarusi
- B. umati wa watu
- C. mapadri
- D. wageni harusini

**47.** Mbona wengi wakapigwa na butwa?
- A. kwa kuona maarusi
- B. kwa kumwona Aisha
- C. Arusi ilifana
- D. kwa sababu ya mwanamke aliyedai kuwa mke wa Juma

**48.** Arusi ilichacha saa ngapi?
- A. asubuhi
- B. adhuhuri
- C. jioni
- D. alasiri

**49.** Wali ni chakula kinachotokana na
- A. mihogo
- B. miwa
- C. mchele
- D. pamba

**50.** Kichwa kifaacho kwenye habari hii ni
- A. Arusi iliyoishia vyema
- B. Siku ya Jumamosi
- C. Arusi iliyotumbukia nyongo
- D. Arusi iliyopendeza



Compiled & distibuted by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi – Nairobi Tel:+254202319748
**E-mail:** infosnkenya@gmail.com | **ORDER ANSWERS ONLINE** at www.schoolsnetkenya.com